# CATHOLIC DIOCESE OF MOSHI

ST. PAMACHIUS INCLUSIVE SECONDARY SCHOOL
P. O. BOX 1303
**MOSHI – TANZANIA**
st.pamachiusinclusive2019@gmail.com


PROT. No. CDM/SPISS/VI-127/2020 ----/----/2020

Mzazi wa ____________________________
S.L.P. ________________
________________________

Mpendwa ________________________________

YAH: MWANAO KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA KIDATO CHA KWANZA 2020

Husika na kichwa cha habari hapo juu.
Ninafurahi kukujulisha kwamba mwanao amechaguliwa kuanza masomo ya Sekondari kwenye Shule ya Sekondari "St. Pamachius Inclusive". Hongera sana!!

Shule itafunguliwa kwa mhula wa kwanza wa masomo Jumatatu, tarehe 06.01.2020. Siku ya kufungua shule Mzazi au Mlezi amlete mtoto shuleni kuanzia saa tatu kamili asubuhi (3:00) hadi saa sita na nusu (6:30) mchana.

Aidha tunakuomba uthibitishe kukubali mwanao kujiunga na shule yetu kwa kulipa shilingi 200,000/- kwenye akaunti ya shule kwa kutumia taarifa zifuatazo:

Jina la Akaunti: 'St. Pamachius Inclusive Secondary School - Fees"
Namba ya Akaunti: 00511503575303
Benki: Mkombozi Commercial Bank
Tawi: Moshi

Risiti ya malipo ya benki iwasilishwe kwenye Ofisi ya Mhasibu shuleni, kabla ya tarehe 12.10.2019. Fedha hizi ni sehemu ya ada ya mwanao kwa mwaka wa masomo 2020.

Siku ya kufungua shule, ufike akiwa na barua hii ya kukubaliwa kujiunga na masomo hapa shuleni pamoja na Fomu yenye Maelezo Muhimu kuhusu Shule, Sheria, Taratibu na Kanuni muhimu za Shule, Fomu ya tadhmini ya Daktari kuhusu afya ya mtoto, na Fomu ya Ahadi ambazo zimeambatanishwa na barua hii.
Kwa niaba ya ungozi wa Jimbo Katoliki Moshi ninakushukuru kwa kuchagua kujiunga na shule yetu. Uongozi wa Shule unaomba ushirikiano wako katika malezi na taaluma ya mtoto wetu ili, kwa msaada wa Mwenyezi Mungu, aweze kufaulu vizuri katika masomo na kufikia malengo yake kimaisha.

Katika Kristo Bwana,

Padre Patrick E. Asanterabi
MKUU WA SHULE

*Ambat:* 4